



WIZARA YA ELIMU,  
SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MoEST Weekly

23 April, 2026



## PROGRAM YA SAMIA YA UTAMBUZI NA URASIMISHAJI UJUZI YAZINDULIWA

“ELIMU NA UJUZI NDIO MPANGO MZIMA”

#ElimuUjuziMpangoMzima

     | [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz)

# PROGRAM YA SAMIA YA UTAMBUZI NA URASIMISHAJI UJUZI YAZINDULIWA

**K**wa mara ya kwanza nchini Tanzania, imezinduliwa Programu ya Mama Samia ya Utambuzi na Urasimishaji Ujuzi, ikilenga kurasimisha maarifa yanayopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu.

Kupitia Program hiyo Serikali inalenga kuwafikia vijana 80,000 ifikapo Juni 2027. Tayari kati ya Aprili 7 - 29, 2026, vijana 14,400 kutoka mikoa 11 wamejiandikisha.

Katika uzinduzi huo Aprili 22, 2026 jijini Dodoma, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amesema mpango huo ni utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, toleo la 2023 na maono ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Aidha, amengeza kuwa, Program hiyo inaenda sambamba na malengo ya Dira 2050 kuifanya Tanzania kuwa na wataalam wa kutosha wenye ujuzi na uwezo wa kuhimili ushindani katika ngazi za kikanda na kimataifa.

“Huduma ya kurasimisha ujuzi itawafuata mafundi mlipo, unachotakiwa ni kuwasilisha maombi ofisi za Halmashauri ama chuo cha VETA kilichopo karibu” Amesema Prof. Mkenda.

Naibu Waziri Mhe. Wanu Hafidhi Ameir amesema kuwa programu itasaidia kuongeza ushindani wa ujuzi na kushirikisha wananchi katika fursa za kiuchumi.

Mkurugenzi Mkuu wa VETA, CPA Anthony Kasore, ameahidi kusimamia kwa karibu utekelezaji wa mpango huu kwa uwazi na weledi.

Baadhi ya wanufaika wa Programu ya Mama Samia ya Utambuzi na Urasimishaji Ujuzi, akiwemo Paulina Chuma na Anthony Kitiani, wameeleza kuwa mpango huo ni daraja la kuingia kwenye fursa kubwa za kiuchumi na kijamii.

